



DHUL HIJJA 1447 HIJIRIA — JUNI 2026 MILADIA (Bei Tsh 4,000/= - Ksh 200/=)

NDIO SULUHISHO

MKUTANO WA 'AFRICA FORWARD': U FARANSA KUGEUKIA NCHI ZINAZOZUNGUMZA KIENGEREZA KUFUFUA USHAWISHI WAKE



Ufaransa liandaa mkutano wa siku mbili wenye anuani : *Africa Forward* (Kusonga mbele kwa Afrika) uliofanyika mnamo tarehe 11–12 Mei 2026 mjini Nairobi (Kenya), ambao ulihitimishwa kwa Azimio la Nairobi lililolenga kuimarisha zaidi mahusiano ya kiuchumi kati ya Ufaransa na Afrika, kutilia mkazo ukuaji wa viwanda, na kuipa Afrika sauti kubwa zaidi katika mifumo ya kifedha na kisiasa duniani.

Mkutano huo ulihudhuriwa na karibu viongozi wa juu 30 wa nchi, mashirika ya kimataifa pamoja na zaidi ya wakurugenzi 1,500 wa biashara na wengineo.

Ufaransa ilitangaza kujifunga kwake kuwekeza dola bilioni 27 (£ bilioni 20) barani Afrika katika sekta kama nishati, teknolojia ya kidijitali, akili bandia (AI), uchumi wa bahari na kilimo.

Rais Macron alisema: “Afrika ndio

bara linaloibuka duniani ... na linahitaji uwekezaji ili liwe huru zaidi.” Akaongeza kwa kusema: “Hatuko hapa tu ili kuwekeza Afrika pamoja nanyi — tunahitaji pia wafanyabiashara wa Afrika kuwekeza Ufaransa.”

Mkutano huo ulikumbana na maandamano ya wapinga ubeberu na wakosoaji, baadhi yao walichoma moto bendera za Ufaransa. Macron pia alizua taharuki ndani ya mkutano huo baada ya kujigamba kwamba Ufaransa ni miongoni mwa “Wana majmui wa kweli wa Afrika” (true Pan-Africanist) Imechukua miaka 10 kwa mkutano wa kwanza wa Ufaransa na Afrika kufanyika nje ya Ufaransa au nchi za Afrika

Inaendelea Uk. 2




Yaliyomo :

- ♦ Tahariri.....2
- ♦ Udh-hiya na Khilafah ?! 3
- ♦ Kipimo cha DNA na utambuzi wa mtoto..... 5
- ♦ Usanii wa kupambana na dawa za kulevya.....6

UKOMAVU WA KISIASA WA UMAR KATIKA SIKU

ZAKE ZA MWISHO

(DHUL HIJJA 23 HIJIRIA)



Siku ya Jumatano mwishoni mwa mwezi wa Dhul Hijja mwaka 23 Hijria, Khalifah Umar ra. alijeruhiwa vibaya kwa dhoruba kali ya upanga wakati alipokuwa akiswalisha swala ya alfajiri.

Dhoruba kali ya pigo la upanga alilopigwa kwa uadui na uovu na Abu Lu'u Lu'u (laana ya Allah iwe juu yake) lilikuwa ni jaribio lililokusudiwa kumuua kabisa, na kwa masikitiko makubwa baada ya siku chache tu alifariki dunia.

Kifo cha Umar ra. kilitokea katika mwezi wa Muharam siku ya Jumapili, siku nne tu baada ya kumalizika mwezi wa Dhul Hijjah akiwa na umri wa miaka 63, kikiacha msiba mkubwa usiomithilika kwa Umma mzima wa Kiislamu.

Khalifah Umar ra. atakumbukwa daima kwa mengi katika Uislamu hususan katika zama za Khilafah yake kuanzia

Inaendelea Uk. 5

zinazozungumza kifaransa. Hii ni hatua ya kutapatapa Ufaransa kujaribu kufufua ushawishi wake nje ya ngome zake za asili. Nafasi ya ushawishi wa Paris imeendelea kudhoofika, , na ngome yake ya ushawishi inapitia mabadiliko makubwa machungu baada ya Ufaransa kutimuliwa na nafasi yake kuchukuliwa na mabavu ya Marekani.

Ufaransa imefukuzwa katika nchi za Afrika zinazozungumza Kifaransa barani Afrika hususan nchi za Sahel, ambako tawala za kijeshi zimewaondoa madarakani viongozi wa kiraia marafiki wa Paris, huku tawala hizo za kijeshi zikielekea kwa Marekani.

Kwa upana, mkutano huu katika nchi inayozungumza Kiingereza (Anglophone) ni juhudi ya Ufaransa kujiokoa baada ya kupoteza ushawishi wake Afrika Magharibi, hasa katika zilizokua ngome zake zenye utajiri mkubwa wa madini kama Mali, Niger na Burkina Faso.

Paris haina budi ila kubuni mkakati wa kuonyesha unyenyekevu wa kinafiki katika maeneo mengine ya Afrika kwa lengo la kuendeleza ukoloni mamboleo, uporaji na unyonyaji wa rasilmali za Afrika.

Hali hii inaonesha kushindwa kwa mfumo wa kibepari pamoja na uroho wake wa kikoloni juu

Inaendelea Uk.8

Huu ndio mwezi wa mwisho wa mwaka 1447 Hijria, naa baada ya mwaka huu, siku chache zijazo InshaAllah tunaanza mwaka mpya wa Kiislamu wa 1448 Hijria.

Hapana shaka kwamba mwaka utabadilika kwa jina na hesabu lakini hali zetu kama Umma bado hazikubadilika, lakini kuna dalili zinazotupasa kuzitafakari na kutusukuma zaidi kuleta mabadiliko

Umma wetu umetoka katika mwaka unaomalizika wa 1447 Hijria kama kawaida katika machungu na maumivu kama unavyotoka kila mwaka tangu kuangushwa dola ya mwisho ya Kiislamu ya Khilafah mnamo mwaka 1342 H/ 1924 M.

Mwaka 1447 Hijria pamoja na mashaka mengine mengi tuliyo-nayo, Umma wetu umegubikwa tena na vita vya Marekani na kibaraka wa Israel dhidi ya Umma wa Kiislamu Iran.

Hapana shaka vita vimetudhuru na vinaendelea kutudhuru kwa kuwa bado kiudhati havijasita lakini tukiwa mwishoni mwa mwaka kuna mambo nyeti kutokana na uvamizi huo ambayo tunapaswa kujifunza, na kutokana nayo yawe dira katika kuanza kwetu mwaka mpya.

Vita vya Marekani kwa Iran vimetuthibitishia pasina shaka udhaifu wa dola ya Marekani

japo tulikuwa tukiliamini hilo, lakini nyoyo zetu zimetulia zaidi, na sio sisi tu bali wanadamu na walimwengu kwa jumla.

Wakati wote tunapozungumzia ufaradhi wa kurejesha Khilafah wapo wenye shaka kwamba Marekani kutokana na nguvu zake ni kizuizi cha kulifikia hilo.

Vita hivi vimeifedhehi Marekani, katika jambo hilo, fedheha ambayo haitozibika kwa makarne.

Fedheha hiyo imekua uwanjani kiasi cha vibaraka katika ulimwengu wa Kiislamu na nchi nyengine kama Korea ya Kusini kujionea wazi wazi kwamba Marekani haina ubavu wa kuwalinda kama walivyofikiria. Itawalindaje ikiwa haiwezi kujilinda nafsi yake?

Aidha, mwaka unaomalizika sio tu tumeona udhaifu wa Marekani bali unyeti wa biladi zetu katika kusafirisha bidhaa mbali mbali kama tunavyoona unyeti wa Mlango wa Hormuz nk.

Matukio hayo dhidi ya Marekani yaupe Ummah wetu msukumo yakiwa bishara njema ya kufuatia ushindi mkubwa wa kurea Khilafah Rashidah, kama alivyohindwa Abraha na jeshi lake ndani ya mwezi wa Muharram kisha ikaibuka nuru ya ujio wa Mtume SAAW.

Mhariri

01 Dhul Hijja 1447 Hijria

Juni 2026 M

jukwalakhilafah@gmail.com

Tunamshukuru Allah Taala kwa kuingia tena katika Siku tukufu ya Eid ul-Udh- hiya. Siku adhimu aliyoiteua Mola wetu kuwa sikukuu kwa Umma wetu mtukufu.

Licha ya Umma wetu kusibiwa na kila aina ya madhila kuanzia vita, mateso, kuekwa vizuizini, umaskini unaosababishwa na vibaraka kwa kuvuruga kwao mali za Umma nk. bado, hatuna budi kumshukuru Allah Taala na kupongezana kwa siku hii. Nasi tunasema Eid Mubarak! kwa Umma wetu mashariki na magharibi.

Eid hii inaambatana na tukio kubwa la muhanga la Nabii Ibrahim (As) kumtoa muhanga mwanawe Ismail As. kwa amri ya Allah Taala. Kwa maneno mengine, hii ni Eid ya kutathmini kiwango cha muhanga wetu katika Uislamu wetu.

Enyi Waislamu,

Hapana shaka muhanga katika dini yetu ni jambo la wakati wote na katika ibada zetu zote, na Alhamdulillah! hatusemi Waislamu hawatoi muhanga. Tunachosema kuna eneo ambalo limesahuliwa kupewa muhanga stahiki au kutopewa kabisa, eneo ambalo ndio mama wa yote katika Uislamu. Nalo ni ulinganizi wa kurejesha tena dola ya Kiislamu ya Khilafah.

Muhanga katika qadhia hii ya kurejesha Khilafah unapaswa uwe kipaumbele wakati wote tena kwa kiwango cha juu, kwa sababu kurejea tena kwa dola hiyo ndio tiba ya yote yanayousibu Umma wetu tangu kuangushwa dola hiyo mnamo mwaka 1342H/1924M. Umma wetu tangu wakati huo umekua ukihangaika na kutangatanga

kwa dhiki na mabalaa bila ya mchungu, mlinzi, utatuzi wala mtezi.

Enyi Waislamu,

Jee mnajua kuwa kuishi zaidi ya siku tatu bila ya Khilafah na kutokea na jitihada ya kuirejesha ni dhambi katika madhambi makubwa(kabaair) ilhali leo tukiwa ndani ya miaka 105 bila ya utawala huo wa Khilafah?

Jee mnajua kwamba Khilafah ni faradhi ambayo masahaba na waliowafuata wao hawakuichel ewesha wala kuizembea hata kwa muda mdogo, kiasi kwamba alipofariki Khalifah mmoja waliweka Khalifah mwengine kwa haraka?

Jee mnajua kuwa kukosekana Khilafah ndio chanzo cha umasikini, uvamizi wa makafiri katika biladi zetu, mateso ya Waislamu Kashmiri, Myanmar, Turkistani Mashariki, kumwagwa damu zetu kwa kutumia ardhi, anga na mali zetu Waislamu kama Gaza, Sudan, Iran, Lebanon nk? Bila ya kusahau namna makafiri wanavyokashifu matukufu yetu kama mayahudi kwa Masjid Aqsa, kutukanwa Allah Taala, Mtume wake SAAW, vitendo vya chuki dhidi ya Uislamu na Waislamu kama tukio la karibu zaidi (ndani ya mwezi huu) la kukashifiwa Quran Marekani kwa kuchomwa na mbaguzi na adui wa Uislamu Jake Lang nje ya Msikti wa Dearborn, Michigan, mauaji ya kigaidi katika masiku haya matukufu dhidi ya Waislamu watatu wasio na hatia yaliyotendwa na wabaguzi Cain Clark (17) Caleb Vazquez (18) katika kituo cha Islamic Centre cha San Diego, Carlifornia nk.

Enyi Waislamu :

Muhanga wa baba wa Mitume (Ibrahim As.) utuzindue kutoka ka

tika usingizi mzito wa kuzembea katika qadhia hii nyeti. Tam-bueni ni kwa Khilafah tu ndio heshima na izza ya Umma wetu itarudi, ibada kama Hija na nyengine zitalindwa na kusimamiwa vyema , utajiri wa Umma utahifadhiwa na kutumika vyema kwa ajili ya raia wa Dola ya Khilafah, maeneo yetu nyeti ya kimkakati kama Mlango wa Hormuz, Mfereji wa Suez, Bab Al-Mandeb nk. yatalindwa kwa nguvu zote, na kamwe 'kafiri harbii' hatokuwa na hata fursa ya kuchungulia. Umma wetu wakati huo utarudi katika umoja wake wa asili chini ya kuvuli cha mtawala mmoja na bendera moja, huku nuru ya Uislamu itaangazia tena kwa Waislamu na walimwengu wote mashariki na magharibi. Basi Enyi Umma wetu mtukufu toeni muhanga wenu kwa kujumuika na wanaharakati wa Hizb ut Tahrir katika qadhia hii adhimu kwa kubeba Da'wa ili kuirejesha Khilafah ya Kilimwengu kwa njia ya Mtume SAW.

Wakullu 'amun wa-antum bikhayr

10 Dhul- Hijja 1447 Hijria/ 27 Mei 2026 Miladi

hizbtz.org



UTAMBUZI WA NASABA YA MTOTO KWA CHEMBE CHEMBE ZA DNA

Swali

Assalamu Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

Sheikh wetu mhashimiwa, Je, mtu aweza kukana nasaba ya mwana-we kutokana na uchunguzi wa vinasaba vya DNA? Baraka za Allah zikushukie

Jibu

Wa Alaikum Assalam Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

Kwanza, kunapotokea hali yoyote ya kutofautiana juu ya kadhia yoyote, inajuzu kutumia njia zozote za sawa za uthibitishaji na kuhakikisha ziko sahihi ... Miongoni mwa njia hizi ni chembe chembe za DNA, na njia za uchunguzi wa kisayansi, na njia zozote za uthibitishaji zitakazo pelekea kupatikana kwa rai sahihi katika kadhia yoyote, isipokuwa kukiwepo na nasi maalumu ya kisheria juu ya kadhia fulani, hapo nasi hiyo inakuwa ni yenye kufunga kwa ukamilifu.

DNA ni sehemu ya maumbile kwa wanadamu na viumbe vyenye uhai. Inajumuisha kanda mbili zilizo unganishwa na kushikamanishwa pamoja mithili ya ngazi. Pambizo zake zinakusanya chembe chembe za sukari aina ya deoxyribose na phosphate, na vipandio vya ngazi hii vinakusanya madini aina ya nitrogen. Hii inamaanisha kuwa kila ukanda unakusanya viwango vya sukari, madini ya phosphate na nitrogen. Kila chembe moja huitwa nucleotide.

Nucleotide hizi zimepangwa imara. Mkusanyiko huu wa kanda za nucleotide umegawanyika katika sehemu kadhaa zinazo itwa genes. Kila gene moja ina sifa



maalumu inayotoa maagizo yanayo hitajika kutengeza aina fulani ya protini; mali ghafi yanayo unda misuli ya mwili.

Genes hizi au "utambulisho wa kigene" hubeba maumbile ya kurithika kwa wazazi na watoto. Ni maumbile yafananayo yaliyo umbwa na Allah (swt) ili kuunganisha kizazi pamoja, ikiwa tutazingatia kinadharia usahihi wa utafiti na usahihi wa matokeo ya DNA kati ya baba na mwanawe, yaani, tupate maalumati ya genes kutokana na utambulisho wa kigene kama ulivyo umbwa na Muumba (swt), kuonyesha kuwa mtoto huyu ni wa baba huyo. Lakini, wajuzi na weledi wanasema kuwa kuna uwezekano wa kutokea kwa dosari katika matokeo ya utafiti kutokana na yanayojiri wakati wa uchambuzi wake, dosari za kibinadamu au za kimaabara, au kuchafuka kwa sampuli, pamoja na 'shauku' juu ya uaminifu wa mwenye kufanya utafiti huo na kujitolea kwake katika tajriba ya utafiti huo pasi na kuathiriwa na dhurufu nyenginezo. Yote haya huathiri matokeo.

Hivyo basi, matokeo ya uchunguzi wa DNA sio lazima yawe ya kukatikwa kwa sababu ya kuwepo kwa uwezekano wa dosari katika matokeo yake kutokana na dhurufu zilizo tajwa juu. Ikiwa dosari hizo zitakabiliwa, matokeo hayo yanaweza kutumi

ka kama uthibitisho kwa kadhia yoyote ile isiyokua na nasi ya kisheria kuithibitisha, lakini kunapokuwa na nasi ya kisheria ni lazima kujifunga nayo kikamilifu.

Kwa mfano, wakati wa kuutambua mwili wa mtu asiyejulikana... au kuthibitisha uzazi wa mama, au kunapo kuwa na sintofahamu mahospitalini... yaweza kuthibitishwa na kuchunguzwa kwa njia yoyote sahihi ya uthibitishaji, na njia yoyote sahihi ya uchunguzi na uthibitishaji ... mithili ya uchunguzi wa DNA, ikiwemo uchunguzi wa makini wa eneo ambalo mwili ulipatikana, pamoja na wahudumu wa wadi ya kujifungulia kina mama hospitalini, na kwa njia nyengine yoyote sahihi ya uthibitishaji, ili kuhakikisha usahihi wa matokeo yaliyo patikana ... Yote haya yanajuzu kwa sababu hakuna nasi maalumu ya kisheria ya kuyathibitisha, na hivyo kuangukia ndani ya sheria jumla. Lakini, kunapo kuwa na nasi ya kisheria kuhusiana na kadhia hii ni lazima kujifunga kwayo pekee.

Pili: Sasa twaja katika swali lako kuhusu kukana nasaba ya mtoto (upande wa baba) ... Kuna nasi ya kisheria kuhusiana na kadhia hii, hivyo basi ni lazima kujifunga kwayo pekee, kama ifuatavyo:

1- Matokeo ya uchunguzi wa DNA hayachukuliwi kama dalili ya kadhia hii, kwa sababu kuthibitisha au kukana nasaba ya

(Inaendelea uk .7)

msimamo wake thabiti katika Uislamu, ujasiri, uadilifu, ucha Mungu na kufanya fat-hi kati-ka maeneo mbalimbali kwa kueneza nuru ya Uislamu mashariki na magharibi kuto-kana na kuandaliwa mazingira mazuri na Khalifah aliyemtangulia Abubakar ra. ambaye kwa bahati mbaya yeye binafsi hakuweza kufungua miji mingi kutokana na kukabiliwa na wimbi kubwa la matatizo ya ndani.

Moja katika tukio kubwa la kihistoria ambalo milele Umar ra. atakumbukwa ni kitendo chake cha ujasiri kinachodhihirisha kupevuka kwake kisiasa kwa kuandaa mazingira mwanana yaliyosahilisha kupatikana Khalifah baada ya kufariki kwake.

Siku chache kabla ya kifo chake katika hali ya kuwa na majeraha makali kama aliyoyapata, Waislamu walimkabili Umar ra. awapendekezee mtu wa kushika wadhifa wa Khilafah baada yake. Umar RA aliwajibu yafuatayo:

'Kama nitamteua mtu baada yangu hakutokuwa na kasoro yoyote katika hilo kwa vile Abubakar aliniteuwa mimi baada yake, nae alikuwa mbora kuliko mimi. Lakini kama sitoteuwa mtu baada yangu, hakutokuwa na kasoro yoyote kwani Mtume wa Allah hakuteuwa mrithi wake, nae alikuwa mbora kuliko sisi sote' (mimi na Abubakar)

Hatimae baada ya maswahaba kumshikilia na kumsisitiza sana awateulie wa kuishika nafasi baada yake kwa kuchelea Umma kusambara

tika na kupelekea kuzuka fujo na vurugu. Umar alimchagua sahaba mashuhuri Suhaib Al- Rum kuwa Amiri wa muda ili asimamie zoezi zima la kumchagua Khalifah kwa kipindi chote cha mchakato wa kumtafuta, pia alimtaka awe imamu wa swala zote za jamaa kwa kipindi chote cha kujeruhiwa kwake, kadhalika alimpa jukumu awe imamu wa jenezake lake lau atafariki dunia. Na zaidi akampa mamlaka yote ya kumtia adabu ya kumkata kichwa yoyote atakaekwamisha zoezi au kuleta upinzani baada ya kupatikana Khalifah.

Kwa hivyo, Umar akawateua masahaba sita mashuhuri: Ali bin Abi Twalib, Uthman bin Affan, Abdulrahman bin Auf, Talha, Zubeir na Saad bin Abi Waqas. Maswahaba hao aliwaweka chini ya usimamizi wa Suhaib kama Amiri wa muda ili mmoja wao awe Khalifah baada yake baada ya kuupitia mchakato wa uchaguzi. Na Umar akawaeleza wazi kwa matamshi ya kihistoria alipotamka:

'Enyi kundi la Muhajirina, hakika Mtume wa Allah alikufa na aliridhika na nyie nyote sita. Nimelifanya suala la Khilafah ni suala la mashauriano miongoni mwenu , ili kwamba murweze kuchagua mmoja miongoni mwenu kama Khalifah. Kama watano miongoni mwenu wakikubaliana juu ya mtu mmoja, na mmoja akapingana nao basi muuweni, kama wanne wakiwa upande mmoja na wawili wakiwa upande wa pili na kupinga, basi wauweni hao wawili, na kama watatu wakiwa upande mmoja na watatu wako upande mwingine basi Abdul Rahman bin Auf atakuwa na kura ya kukata shauri na Khalifah atachaguliwa kutoka kundi lake, katika hali kama

hiyo wauweni watatu waliobaki lau watapinga kwa kuleta upinzani'. (Tariukh- Twabbary) Baada ya kufariki Umar ra. na kufuatia mchakato aliouweka wa kutafutwa Khalifah baada yake, Waislamu kwa umoja wao waliwafikiana kumchagua Uthman bin Affan ra. kuwa Khalifah baada ya Umar na akapewa rasmi bai'ya/ kiapo cha utii na Waislamu na akashika hatamu za uongozi wa dola ya Kiislamu.

Katika qadhia hii tunajifunza namna Waislamu wa wakati huo walivyojengeka katika upeo wa hali ya juu kabisa kati-ka siasa za Kiislamu. Siasa zilizozongozwa na fikra sahihi za Kiislamu, kiasi kwamba wakati wote Umma ulihisi uhai wake unapokuwa unasimamiwa mambo yake na kiongozi wa Kiislamu ambaye ni Khalifah na kamwe hawakuruhusu Umma ubakie bila ya mchungu kama hali yetu tulivyo leo.

Ni Umma ndio uliomtaka Umar ra. aandae kupatikana kiongozi baada yake, nae akachukua jukumu hilo kwa kumteua Amiri wa muda kusimamia mchakato mzima wa kuteua Khalifah mpaka kukamilika kwake. Ufahamu huo unatoka-na na msingi kabambe na thabiti alioutandika Mtume SAAW.

Ktendo cha kutoa bai'ya kwa Khalifah ni wajibu, lakini wajibu huo hauwezi kutekelezeka ila kwa kupatikana Khalifah, hivyo ni jukumu la Umma kumtafuta Khalifah ili uweze kutekeleza amri hii.

VITA VYA KISANII DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA

Kimataifa kila tarehe 26 Juni ni Siku ya Kupambana na Biashara na Matumizi Haramu ya Dawa za Kulevya Duniani. Siku hii ilichaguliwa na Baraza Kuu la Umoja mwaka 1987.

Maadhimisho hayo hulenga na kuhamasisha jamii, hasa vijana, kujiepusha na vishawishi vya dawa za kulevya, kuimarisha ushirikiano wa kimataifa, kikanda, na kitaifa katika kukabiliana na usafirishaji haramu wa madawa hayo, kutoa Msaada katika juhudi za kuwatibu, kuwahudumia, na kuwajumuisha upya katika jamii waathirika nk.

Umoja wa Mataifa umeunda taasisi maalumu inayoitwa **United Nations Office on Drugs and Crime (UNODC)** wakidai inakabiliana na matumizi na biashara ya madawa ya kulevya, huku nchi mbali mbali kwa agizo la kimataifa zina taasisi za kupambana na tatizo hilo, na kwa upande wa Tanzania mapambano dhidi ya madawa ya kulevya huongozwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), kwa ku-shirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo vyombo vya ulinzi na usalama.

Ni ukweli usiopingika kwamba dawa za kulevya huwafanya watu wengi kuwa wahanga kupitia uraibu na biashara hiyo haramu. Kwa mujibu wa ripoti mpya ya Umoja wa Mataifa kuhusu dawa za kulevya duniani, idadi ya watumiaji wa dawa hizo imeongezeka hadi milioni 29 kutoka milioni 27 katika miaka ya karibuni.

Tanzania pekee ina zaidi ya wasafirishaji 1,000 wa dawa za kulevya walioko katika magereza ya nchi



za kigeni, huku 68 kati yao waki-hukumiwa adhabu ya kifo nchini China, bila kusahau maelfu ya waraibu wa ndani ya nchi.

Itakumbukwa pia aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Paul Makonda katika mwezi wa Februari mwaka 2017 aliwataja baadhi ya wafanyabiashara maarufu, viongozi wa dini, wanasiasa, watu mbalimbali maarufu pamoja na maafisa wa polisi kuwa miongoni mwa watuhumiwa wanaohusishwa na biashara hii haramu.

Matajiri wa biashara ya dawa za kulevya wameenea duniani kote wakifurahia biashara yenye faida kubwa inayochukuliwa kuwa biashara ya tatu kwa faida kubwa duniani baada ya biashara ya mafuta ya petroli na silaha.

Mnamo mwaka 2011, tovuti ya Wikileaks ilifichua majina ya wanasiasa mbalimbali maarufu waliokuwa wakijihusisha na biashara ya kimataifa ya dawa za kulevya kwa kutumia nafasi zao za juu serikalini. Pia yapo madai kutoka kwa waandishi mbalimbali kuhusu kuhusika kwa CIA katika biashara ya usafirishaji wa dawa za kulevya.

Kwa kawaida, biashara hii haramu huwa ina mtandao mkubwa na hushirikiana na magenge maalumu ya uhalifu, wafanyabiashara wakubwa pamoja na maafisa muhimu wa serikali ili kufanikiwa. Hali hii hufanyika kupitia njama za kiwango cha juu zinazohusisha polisi, vyombo vya ujasusi vya taifa,

maafisa wa bandari na viwanja vya ndege na wengineo.

Kimsingi, duniani kote haku-na mfanyabiashara mkubwa wa dawa za kulevya anayekamatwa isipokua wauzaji wadogo wadogo kwa ajili ya kuonyesha mapambano ya kinafiki yenye lengo la kuwadanganya wananchi huku biashara yenyewe ikiendelea kukua zaidi. Ukiangalia kwa makini kinachoitwa vita dhidi ya dawa za kulevya, utagundua kuwa biashara hiyo imekuwa ikiongezeka zaidi kutoka miongo hadi miongo.

Mabepari na wafuasi wa mfumo wa kisekula hawawezi kuzuiya kasi ya biashara hii ya kihalifu badala yake wanaikuza na kuiendeleza. Mfumo wa kidemokrasia na kibepari huangalia kila kitu kwa jicho la faida huku ukipuuza madhara mengine yanayotokea. Pia mfumo huu hutukuza “uhuru” wa kufanya chochote katika kila nyanja ya maisha, huku maana ya furaha ikielezwa kuwa ni kutosheleza matamano ya kimwili kwa mujibu wa tamaa zisizo na mipaka. Ndiyo maana biashara ya dawa za kulevya, matumizi yake pamoja na biashara ya pombe huzidishwa kila siku.

Kwa kuwa nchi changa zinai-ga mfumo wa kibepari ambao msingi wake ni faida na maslahi, wanasiasa hawawezi kwa namna yoyote kujitenga na wakubwa wa kisiasa duniani wanaohusika katika

Inaendelea uk. 7

biashara hii. Hivyo basi, hatua zinazochukuliwa kupambana na dawa za kulevya ni kauli tupu zisizo na ukweli, bali ni njia ya kuendeleza biashara hiyo.

Aidha, wanatumia suala hili la madawa ya kulevya kama kisingizio na mbinu ya kisiasa ya kuwapotosha wananchi kutoka katika matatizo ya sasa ya kiuchumi kama njaa, ukosefu wa ajira, kufeli kwa wanafunzi wengi katika mitihani ya sekondari nk.

Uislamu kama mfumo kamili wa maisha unaotekelezwa kupitia dola ya Khilafah utaikomesha biashara ya dawa za kulevya, pombe na biashara nyingine zote zenye mahusiano nayo, kwa kuwa ulevi wote ni haramu katika Uislamu. Allah Taala anasema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ
وَالْأَزْلَامُ رَجَسٌ مِنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ
تُفْلِحُونَ (المائدة: 90)

Enyi Mlioamini!Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa [kuomba] asiyekua Mwenyezi Mungu,na kupiga ramli,[yote haya] ni uchafu [ni] katika kazi za shetani. Basi jiepusheni navyo,ili mpate kufaulu.

Aidha, Mfumo wa Uislamu kamwe hautatangulizi faida mbele ya maisha ya watu, bali utatumia msingi wa 'halali' na 'haramu' katika miamala yote.

Na kuhusu furaha na utulivu wa moyo, hayo yatapatikana kwa kushikamana na amri za Mwenyezi Mungu na kuamini qadhaa na qadar, bila kuhusisha matumizi ya dawa za kulevya.

Zaidi ya yote dola ya Kiislamu ya Khilafah itatoa adhabu kali

kwa kila anaejijhusisha na utumiaji, usambazaji na wenye kujihusisha na biashara hii ya kihalifu.

DNA....kutoka uk 4

mtoto kwa mume kuna dalili yake katika Uislamu, nasaba haithibitishwi au kukanushwa pasi kwayo, na fatwa zilizotolewa baada ya kusambazwa kwa utafiti wa DNA haziathiri hili. Fatwa hizi kutoka taasisi za utoaji fatwa, hususan nchini Misri na kamati za Waqf, au nchini Kuwait, zenye rai kadha wa kadha kuhusu kadhia hii. Baadhi yazo zinaruhusu utumiaji uchunguzi wa DNA katika kuthibitisha na kukanusha nasaba, na baadhi zinaruhusu utumiaji wake katika kukanusha pekee na wala si katika kuthibitisha. Baadhi yao zinaruhusu katika uthibitishaji wa nasaba iwapo kuna uhusiano wa kindoa, lakini kutoruhusu kutumiwa katika hali ya uzinifu, na baadhi ya waliolemazwa na thaqafa ya kimagharibi wameruhusu kutumiwa hata katika uthibitishaji wa nasaba katika hali ya uzinifu!!

2- Hukmu sahihi juu ya kadhia hii ni ile ambayo sheria imeifanua makhsusi kuhusiana na nasaba, na tumeieleza katika kitabu cha Nidhamu ya Kijamii, katika mada ya nasaba: "Kuhusiana na mume, pindi mkewe anapojifungua mtoto atahesabiwa anatokana na yeye ikiwa atakuwa amejifungua baada ya zaidi ya miezi sita kuanzia tarehe ya ndoa. Mtoto huyo atakuwa ni wake kutokana na Hadith ya Mtume SAAW: «"Mtoto ni wa mwenye kitanda alichu zaliwa"[IBukhari na Muslim). Kwa ufupi, maadamu mwanamke ni mke wa huyo mume na amejifungua baada ya miezi sita tangu ndoa

bila shaka ni mtoto wa mumewe.

Lakini,hata mke awe amejifungua baada ya miezi sita na mume akawa na hakika kuwa mtoto si wake, inaruhusiwa mume kumkataa kwa masharti maalumu. Kama hakutimiza masharti hayo mtoto atabakia kuwa ni wake, apende asipende. Masharti haya ni:

Kwanza: Mtoto anayemkataa ni lazima azaliwe akiwa hai. Hawezi kukataa nasaba ya mtoto ikiwa amezaliwa akiwa maiti kwa kuwa hakuna hukmu ya kisheria kuhusiana na kumkataa mtoto aliye zaliwa maiti.

Pili: Iwe baba hajakiri ima wazi wazi au kwa siri, kuwa mtoto huyo ni wake. Ikiwa ashakiri wazi wazi au kwa siri kwa kuashiria kuwa mtoto huyo ni wake, baada ya hapo si halali tena kumkana.

Tatu: Kumkana mtoto kuwe ndani ya wakati na hali fulani. Wakati wa kujifungua au wakati wa kununua vitu muhimu vya mtoto, au wakati alipogundua kuwa mkewe amejifungua. Nasaba ya mtoto haiwezi kukanwa nyakati nyengine zozote zisokuwa hizi. Mkewe anapojifungua mtoto na akabakia kimya, bila ya kumkana ingawa alikuwa na fursa ya kufanya hivyo, basi nasaba yake itanasibishwa na yeye na kamwe hatakuwa na haki ya kumkana baada ya hapo. Chaguo hilo linategemea kulingana na mahali alipogundua uwezo wake

Uk.8

ya rasilimali za mataifa ya-nayoendelea.

Zaidi ya yote, hali hii ni aibu kwa Ummah wetu ambao umebarikiwa kuwa na na mfu-mo mbadala madhubuti wa Kiislamu unaoweza kimsingi kusimamisha na kuung'oa kabisa ubepari pamoja na un-yonyaji wake katika ardhi za Waislamu na nyenginezo. Ku-kosekana Uislamu chini ya dola ya Khilafah kumezifanya baadhi ya nchi zinazoendelea kunyenyekea kikamilifu mbele ya madola ya kikoloni — wakati mwengine si kwa hiari, bali wa-kati mwengine ni kutokana na masharti magumu wanayolazimishwa au kutokana na kutokuwepo dola mbadala yenye nguvu ya wao kui-tegemea.

Wakati madola ya kikoloni ya kibepari yanaendelea kuonye-sha kila dalili za kudhoofika, ni wakati muwafaka kwa Waislamu kuirejesha tena dola ya Khilafah Rashidah ili kuukomboa Ummah wa Kiislamu pamoja na mataifa dhaifu yanayoendelea.

MasoudMsellem

**Mwakilishi wa Vyombo vya
Habari wa Hizb ut Tahrir Tan-
zania**

wa kumkana mtoto huyo. Iki-wa alijua kuhusu mtoto huyo na akawa na uwezo wa kumkana na hakufanya asaba ya mtoto huyo itabakia thabiti kwake kwa sababu nasabu ya mtoto ni kutokakitanda ali-chozaliwa kama tulivyotaja Hadithi awali.

Nne: Ukanaji mtoto una-paswa kufuatiwa na kiapo cha *Li'aan*. Mtoto huyo ha-takanwa na yeye isipokuwa kupitia ulaji kiapo hicho. Pin-di masharti haya manne yan-apotimizwa, hapo mtoto huyo atakuwa amekataliwa na kupewa mama yake. Ibn Umar ameripoti kwamba:

"Mtu mmoja alikula kiapo cha Li'aan dhidi ya mkewe zama za Mtume (saw) na kumkana mtoto wake, Mtume (saw) akamtenganisha naye na kumpa mtoto mkewe mto-to."[Bukhari]

Neno Li'aan (kiapo cha kukashifu) limetokana na ne-no laana kwa sababu kila mmoja katika wanandoa anamlaani mwenziwe (katika mara ya tano ya ulaji kiapo hicho) ikiwa mume au mke atakuwa anasema urongo. Chimbuko la hili ni maneno yake Allah (swt) katika Surat Nuur aya ya 6-9 Ikiwa masharti haya ya kumkana mtoto hayatatimizwa basi ha-takanwa na nasaba yake itabaki ubabani, na atabeba majukumu yote kisha-ria.Hivyo basi, nasaba

ya mtoto haikanushwi kupitia uchun-guzi wa DNA bali hukanushwa pekee kulingana na masharti yaliyowekwa na sheria yaliyo tajwa juu.

Tano: Uislamu unachunga sana nasa-ba, na miongoni mwa nasi zake ni: kutoka kwa Sa'ad (ra) kwamba ames-ema, nilimsikia Mtume (saw) akisema:

»"Yeyote anaye jinasibisha na mtu asiye kuwa babake (halisi), na huku anajua siye babake (halisi), Pepo imeharamishwa kwake!" (Bukhar)

Ibn Maja amepokea kutoka kwa Ab-dullah ibn Amr kwamba amesema, Mtume wa Allah (saw) amesema:

"Yeyote anaye jinasibisha na mtu asiye kuwa babake (halisi), hatasikia harufu ya Pepo; na hakika harufu yake husikika umbali wa masafa ya miaka mia tano."

Imepokewa kutoka kwa An-Nassa'i katika As-Sunan Al-Kubra kutoka kwa Abu Huraia, kwamba alimsikia Mtume (saw) akisema:

"Tangu Ayah ya Li'aan ilipoteremka: mwanamke yeyote atakaye mnasi-bisha mtoto na watu wasiokuwa na-saba yake, hatakuwa na chochote kwa Allah, na wala Allah hatamuingiza Pepo Yake, na mwanamume yeyote atakaye mkana mtoto wake, na huku anajua fika kuwa ni wake, Allah ata-muondolea rehema yake, na at-amfedhehesha mbele ya watu wote wa mwanzo na wa mwisho."

Ndugu yenu,

Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah

Amiri wa Hizb ut Tahrir

**7 Rabi' al-Akhir 1439 H
25/12/2017 M**
